



ni kina nani hao?” Alisema, “Watakuwa wanatoka miongoni mwetu na watazungumza lugha yetu.” Nikasema, “Waniamrisha nini lau hali hiyo itatokea katika uhai wangu?” Alisema, “Kuwa pamoja na kundi la Waislamu na Imam (mtawala) wao.” Nikasema, “Lau hakutakuwepo na kundi la Waislamu wala Imam (mtawala)?” Alisema, “Basi jitenge mbali na makundi yote hata kama itakubidi ung’ate (ule) mizizi ya mti mpaka kufa kwako ilhali umebakia katika hali hiyo.” [Sahih al-Bukhari 7080].

Hakika, aya na hadith hizo zinatupa jibu ni kwamba inatustahiki sisi Waislamu kuwa katika hali hii ya maangamivu duniani kote kwa sababu ya udhaifu (wahn) wetu kama inavyohibitishwa:

**Kwanza**, sisi sio tena watumwa kwa Mwenyezi Mungu (swt) badala yake; ni watumwa kwa Wamagharibi wakoloni. Kwa kujifunga na itikadi yao ya kisekula, mfumo wake wa kirasilimali, nidhamu zake na maadili yake. Kwa upande mwingine, tumetupilia mbali itikadi (*aqeedah*) yetu ya Kisiasa ya Kiislamu

**Pili**, tumekubali na tunaendelea kupigia debe fahamu za kukanganya za kisekula za kirasilimali kama vile uzalendo na utaifa yote eti kwa ajili ya kujikurubisha na mujtama ilhali tumelitupa fungamano na umoja wa Kiislamu.

**Tatu**, tumewachukua wasioamini (*makafiri*) kuwa ndio wandani na viongozi wetu dhidi ya Mwenyezi Mungu (swt), Mtume wake (saw) na waumini ambao wanalingania kujisalimisha kikamilifu kwa Shari’ah. Hivyo basi, tunashiriki katika vikao vyao ili kupanga njama dhidi ya Uislamu na Waislamu.

**Nne**, dhamira yetu katika haya maisha ya mpito ya dunia imejikita katika *msingi wa lengo huhalalisha njia*. Hivyo basi, tunajituma usiku na mchana ili kufaulu hapa duniani lakini kwa gharama ya kuikosa Akhera ya milele! Tumefungamanisha kufaulu na kukusanya utajiri wa kimada na kujifurahisha kihisia. Haishangazi kuona kwamba tumeporomoka kiwango cha wanyama.

Kwa kutamatisha, yote yanategemea na chaguo la mtu binafsi ima kubakia katika hali ya udhaifu au kukumbatia matumaini. Mwenyezi Mungu (swt) alisema: ﴿إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ﴾ **“Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo nafsini mwao.”** [Al-Rad: 11].

Njia pekee ya kuthibitisha kuwa hakika umekumbatia matumaini, ni kwa kujitoa katika minyororo ya ubwana wa Wamagharibi wakoloni. Kwa kutupilia mbali itikadi yao ya kisekula, mfumo wao wa kirasilimali, nidhamu zao na maadili yao. Kisha kupatiliza ulinganizi wa kurudisha tena maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Serikali ya Kiislamu ya kweli kwa maana Khilafah kwa njia ya Utume.

Kwa kuwa na /kukumbatia matumaini, inamaanisha kutumia juhudi zako za mwisho (kimada au vinginevyo) katika kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu (swt) kupitia kujiunga na harakati za kunyanyua utambuzi na maoni ya umma na kuwahesabu watawala Waislamu ndani ya ulimwengu wa Waislamu. Kwamba watawala Waislamu waivunjilie mbali mipango ya Sykes-Picot ambayo iliigawanya dola yetu iliyokuwa Dola Moja ya Khilafah na kuwa vijidola vilivyo na mipaka ya kikoloni na ambayo imesababisha maafa tangu kubuniwa kwao. Hivyo basi, ima waukubali Uislamu ndio msingi wa serikali zao na watawale kwa Shari’ah; au wapinduliwe na nafasi zao zichukuliwe na Muislamu mwanamume kama Khalifah. Hakika, ni kwako wewe ima kuzama ndani ya wahn (kuipenda dunia na kukichukia kifo) au matumaini.

Mwenyezi Mungu (swt) alisema: ﴿وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ﴾ **“Na atakaye fanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walio amini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.”** [Al-Maidah: 56].

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro (Abu Taqiuddin)**

**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**